HOTUBA YA MHESHIMIWA JAJI (R) SEMISTOCLES S. KAIJAGE - MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI, KWENYE MKUTANO WA TUME NA VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA UNAOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA RUAHA – JULIUS NYERERE INTERNATIONAL CONVENTION CENTRE DAR ES SALAAM TAREHE 07 JANUARI, 2018

- **Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**
- **Waheshimiwa Wajumbe wa Tume,**
- **Mheshimiwa Msajili wa Vyama vya Siasa,**
- **Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**
- **Mwakilishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu,**
- **Ndugu Mkurugenzi wa Uchaguzi,**
- **Mkuu wa Jeshi la Polisi,**
- **Ndugu Watendaji wa Tume,**
- **Ndugu Waandishi wa Habari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

Bwana Asifiwe!!!, Tumsifu Yesu Kristu!!!, Mwanakondoo Ameshinda!!!, Assalam Aleykum!!!.

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Kwanza, naomba kuchukua fursa hii, kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, niwakaribisheni wote katika mkutano huu muhimu ambao madhumuni yake ni kupeana taarifa na kujadiliana mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Maandalizi ya Uchaguzi Mdogo wa Wabunge kwenye Majimbo Matatu ya Uchaguzi na

Madiwani katika Kata 6 za Tanzania Bara. Ni ukweli kwamba, mnayo majukumu mengi ambayo ni muhimu lakini pamoja na majukumu hayo mmeitikia wito wetu kuhudhuria mkutano huu. Maana bila ya nyinyi kufika Mkutano usingekuwepo. Sisi kama Tume tunathamini sana kuwepo kwenu hapa.

Pili, ningependa nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa kwa namna ambavyo mmekuwa mkitoa ushirikiano kwa Tume nyakati zote, na niwaombe muendelee kuonesha ushirikiano huo, nasi Tume tunawaahidi kuendelea kutoa ushirikiano wakati wote wa utekelezaji wa shughuli zote za kiuchaguzi ikiwa ni pamoja na shughuli zinazohusu Uandikishaji wa Wapiga Kura zinazofanywa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu.

***Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa*,**

Kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 37 (1)(b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, ni jukumu la Tume kusimamia, kuendesha na kuratibu uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Napenda kuwataarifu kuwa, tumepokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 37 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 aliitaarifu Tume juu ya uwepo wa nafasi wazi za Ubunge kwenye Jimbo la Singida Kaskazini lililoko kwenye Mkoa wa Singida na Jimbo la Songea Mjini lililoko kwenye Mkoa wa Ruvuma.

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 113(1), cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume ilipokea hati kutoka Mahakama Kuu ya Tanzania ikithibitisha kuwa Jimbo la Longido Mkoa wa Arusha lipo wazi kufuatia maamuzi ya mahakama hiyo kutengua ushindi wa Ndugu Onesmo Ole Nangole aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo.

Pia, tumepokea barua kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ambaye kwa mujibu kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, alitoa taarifa ya uwepo wa nafasi wazi za Madiwani Katika Kata 6. Kata hizo ni; Keza-Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, Kimandolu-Halmashauri ya Jiji la Arusha, Kurui-Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Bukumbi-Halmashauri ya Wilaya ya Tabora (Uyui), Kwagunda-Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe na Kihesa-Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.

Ningependa kuwatanabahisha kwamba, maandalizi kwa ajili ya uchaguzi kwenye Majimbo hayo Matatu na Kata Sita yamekamilika. Uchaguzi kwenye Majimbo na Kata tajwa utafanyika tarehe 13 Januari 2018.

Vivyo hivyo, Tume ingependa kutoa Taarifa kwenu kuwa imepokea barua kutoka kwa Mhe. Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, wote wakiitarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Ubunge katika Majimbo ya Uchaguzi ya Kinondoni na Siha pamoja na za Udiwani katika Kata za Isamilo- Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Manzase- Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Madanga- Halmashauri ya Wilaya ya Pangani na Kimagai- Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.

***Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa*,**

Tume imeshawataarifu na kutoa taarifa kwa umma Kalenda ya Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika majimbo ya Kinondoni na Siha na Udiwani katika Kata za Isamilo, Manzase, Madanga na Kimagai.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, utoaji wa Fomu utafanyika tarehe 14 hadi 20 Januari, 2018, uteuzi utakuwa tarehe 20 Januari, 2018, Kampeni zitafanyika kuanzia tarehe 21 Januari, hadi 16 Februari, 2018 na siku ya Uchaguzi ni tarehe 17 Februari, 2018 siku ya Jumamosi.

Tume imeshakamilisha maandalizi yote muhimu ikiwa ni pamoja na kufanya uteuzi wa Wasimamizi wa Uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo na Kata na inatarajia kuendesha mafunzo kwa watendaji hao kuanzia tarehe 09 Januari, 2018.

***Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa*,**

Hadi kufikia leo tarehe 07 Januari, 2018 hatua zifuatazo kuelekea Uchaguzi mdogo wa Wabunge na Madiwani zimechukuliwa;

i. Mafunzo kwa Wasimamizi wa Uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi pamoja na Maafisa wa Uchaguzi wapatao 168 yalifanyika kuanzia tarehe 7 hadi 9 Desemba, 2017 mjini Dodoma. Mafunzo haya yalikuwa ni sehemu ya kuwajengea uwezo wa kusimamia uchaguzi kwa weledi.

ii. Uteuzi wa wagombea ulifanyika tarehe 18 na 20 December, 2017 na rufaa zote dhidi ya maamuzi ya Pingamizi mbalimbali zilizowasilishwa Tume zimeshughulikiwa na kukamilishwa. Aidha, tangu tarehe 19 Desemba, 2017 hadi sasa Kampeni za Uchaguzi zimeendelea kuratibiwa katika maeneo mbalimbali yenye uchaguzi.

iii. Maandalizi ya Vifaa vyote vya uchaguzi yamekamilika kwa asilimia kubwa, na vingi kati ya vifaa hivi tayari vimepelekwa kwenye maeneo yote yenye uchaguzi.

***Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa*,**

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura litakalotumika katika Uchaguzi huu Mdogo ni lile lililotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Hivyo, watakaopiga Kura ni wale tu waliojiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga kura wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Vituo vya kupigia kura, pia ni vile vile vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Vituo hivi vya kupigia kura havitakiwi kuwepo kwenye Ofisi za Chama chochote cha Siasa, majengo ya Ibada, Vituo vya Polisi, nyumba wa majengo ya viongozi wa Vyama vya Siasa.

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Tume iko katika maandalizi ya awali ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Kwa maneno mengine, tangu kukamilishwa kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Tume haijaboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Kutokana na sababu hiyo, Tume kwa kuzingatia matakwa ya vifungu vya 13(2) na 61(3)(a) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi vikisomwa pamoja na kifungu cha 62(a) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, imeruhusu Wapiga Kura walioandikishwa mwaka 2015 ambao ama kwa bahati mbaya wamepoteza Kadi zao za kupigia Kura au Kadi zao zimeharibika au zimechakaa watumie mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo watakapokwenda Kupiga Kura; Kitambulisho cha Taifa, Pasi ya Kusafiria au Leseni ya Udereva.

Ili Mpiga Kura aliyepoteza kadi yake ya kupigia Kura, au Kadi yake imeharibika au kuchakaa aweze kuruhusiwa kutumia vitambulisho vilivyoruhusiwa na Tume, ni sharti awe aliandikishwa kwenye Daftari la Wapiga Kura mwaka 2015, jina lake liwe katika orodha ya Wapiga Kura katika kituo anachokwenda kupiga Kura na majina yake yaliyopo katika Daftari yafanane kwa herufi, maneno na tarakimu na majina yaliyopo katika kitambulisho atakachotumia badala ya Kadi ya kupigia Kura.

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Kwa mujibu wa Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Vyama vya Siasa na Serikali tulisaini kuyakubali na kuahidi kuyaheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi. Ili kuweza kutekeleza Maadili

hayo, Kamati za Maadili za ngazi ya Kata na Jimbo zimeundwa tayari katika maeneo yote yatakayohusika na Uchaguzi mdogo.

Jukumu la Kamati hizi ambazo wajumbe wake ni pamoja na wanachama wa Vyama vya Siasa vyenye wagombea kwenye ngazi ya Kata na Jimbo husika ni; kupokea, kusikiliza, kujadili na kuamua malalamiko ya uvunjaji wa Maadili utakaoweza kufanywa na ama Tume, au Serikali au Mgombea au Vyama vya Siasa au Mwanachama wa chama cha Siasa.

Niwasihi sana kufanya Kampeni kwa kuzingatia Maadili hayo na pale panapotokea ukiukwaji au uvunjaji wa Maadili, Chama au Mgombea awasilishe malalamiko hayo mbele ya Kamati husika kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa kwenye Maadili ya Uchaguzi.

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Tukumbushane; Kama ambavyo Tume imekuwa ikisisitiza katika mikutano yake kama huu wa Wadau Wakuu, napenda kusisitiza kuwa Uchaguzi huu mdogo ambao Kampeni zake zinaendelea utasimamiwa na utaendeshwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria za Uchaguzi na Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hizo, Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2015, maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria nyingine za Nchi.

Hakuna aliye juu ya Sheria hizi na Maadili haya ya Uchaguzi. Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Serikali, Vyama vya Siasa, Wagombea na Wananchi kwa ujumla, tunapaswa kufuata matakwa na masharti ya Sheria hizi za Nchi na Kanuni za Maadili ya Uchaguzi.

Uzoefu katika Chaguzi zilizopita umeonyesha kuwa Vyama vya Siasa na Wagombea wamekuwa wakifuata vyema taratibu zilizowekwa chini ya Sheria za Uchaguzi katika hatua ya Uteuzi wa Wagombea. Katika hatua za Kampeni, upigaji kura, kuhesabu kura, kujumlisha kura na baada ya kutangaza matokeo baadhi ya Vyama vya Siasa na Wagombea wao mara kadhaa wameshindwa

kufuata taratibu zilizoainishwa katika Sheria za Uchaguzi na Maadili ya Uchaguzi hususani pale ambapo Viongozi wa Vyama vya Siasa au wagombea wanaona kuna haja ya hatua zichukuliwe dhidi ya uvunjwaji wa Sheria, Kanuni au Maadili ya Uchaguzi na/au taratibu za Uchaguzi.

Tume inachukua fursa hii kuwakumbusha Viongozi wa Vyama vya Siasa kuwa kwenye Maadili ya Uchaguzi, Sheria za Uchaguzi na kwenye Sheria nyingine za Nchi umewekwa utaratibu fasaha wa jinsi na namna ya kushughulikia malalamiko yanayohusu na kugusa ukiukwaji wa Sheria, taratibu na Maadili ya Uchaguzi ikiwa ni pamoja na kuainisha adhabu na hatua mbalimbali za Kisheria na Kikanuni dhidi ya mgombea yeyote, Chama chochote, Afisa wa Uchaguzi yeyote na hata kwa mwananchi yeyote anayekiuka Sheria za Nchi au Maadili ya Uchaguzi.

Aidha, Sheria na Kanuni za Uchaguzi zimeweka mamlaka na taratibu za kushughulikia malalamiko ya ukiukwaji wa Sheria, taratibu na Maadili ya Uchaguzi. Kwa kuzingatia ukweli huu, Tume inaviasa Vyama vyote vya Siasa na wafuasi wao kutopendelea utaratibu wa kutafuta ufumbuzi wa Kiutawala kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika mambo au masuala ambayo Tume haina mamlaka nayo na ambayo utatuzi wake unahitaji kufuata taratibu za Kisheria na Kikanuni. Umuhimu huu umewekwa bayana kwenye kipengele cha 2.3(e) cha Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2015 ambacho pamoja na mambo mengine kinasisitiza kwamba:

> ”........... *Aidha, malalamiko yeyote yafikishwe kwenye mamlaka inayohusika kwa utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Sheria*”.

Tume ya Uchaguzi inashauri kwa mara nyingine kuwa ni vyema Vyama vya Siasa, kwa kadri inavyowezekana, vitumie utaratibu uliopo wa Kisheria na

Kikanuni katika kuwasilisha malalamiko yanapojitokeza wakati wa Kampeni, kabla na baada ya kuhesabu kura na baada ya matokeo ya kura kutangazwa.

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Kwa mujibu wa kifungu cha 51 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, kikisomwa pamoja na kifungu cha 53 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Tume inayo mamlaka ya kuruhusu kuwepo kwa Kampeni za Uchaguzi katika maeneo ya Uchaguzi. Hivyo, kampeni hizo zifanyike kwenye Majimbo na Kata husika na inategemewa kuwa Mikutano ya Kampeni italenga kuwashawishi, kwa namna ya kistaarabu, wananchi wa Majimbo na Kata husika ili wamchague Mgombea anayefanyiwa kampeni.

Vivyo hivyo; kwa mujibu wa kipengele cha 2.1(c) cha Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2015 tunategemea kila Chama cha Siasa kiendelee kufanya Kampeni kwa mujibu wa ratiba. Kampeni zote zinatakiwa kuanza saa 2:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.

Aidha, Vyama vyote vya Siasa vinakumbushwa kuzingatia Kanuni za Maadili ya Vyama vya Siasa za mwaka 2007 zilizotungwa chini ya Kifungu cha 22(h) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258.

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Kwa kuzingatia matakwa ya vipengele vya 3.2 (a)(b) na 3.3 vya Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2015, Tume imekwisha kutoa ushauri kwa Viongozi wa Mikoa na Wilaya ili katika kipindi hiki cha Uchaguzi wahakikishe wanazingatia wajibu wao na ukomo wa madaraka yao katika shughuli za Uchaguzi kuanzia kipindi cha Kampeni hadi kutangazwa kwa Matokeo.

Aidha, Serikali kwa mujibu wa Kipengele 3.1 (b) cha Maadili ya Uchaguzi inayo wajibu wa kuhakikisha kuwa kuna hali ya Usalama, Amani na Utulivu katika kipindi chote cha Uchaguzi. Kwa maana hiyo, vyombo vya Ulinzi na Usalama vinatakiwa kutelekeza wajibu wake katika kipindi chote cha Uchaguzi kwa kuzingatia kipengele 3.2 (a) cha Maadili ya Uchaguzi.

Vivyo hivyo, watendaji wote wa Uchaguzi wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kwa mujibu wa kipengele 4.2 (a) cha Maadili ya Uchaguzi, bila ubaguzi au upendeleo wa Chama chochote cha Siasa.

***Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa*,**

Mwisho, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuwa Vyama vya Siasa vitakavyoshiriki katika Uchaguzi huu Mdogo pamoja na wadau wengine wataheshimu, watazingatia na kutekeleza Sheria, Kanuni na Taratibu za Uchaguzi, Maadili ya Uchaguzi, maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Sheria zingine za nchi katika kipindi chote cha Uchaguzi.

Tume kwa upande wake imejiandaa vyema kuhakikisha kuwa shughuli zote za Uchaguzi huu mdogo wa Ubunge na Madiwani zinafanyika vizuri na kwa kuzingatia muda uliopangwa ikiwa ni pamoja na kufikisha vifaa vya Uchaguzi katika maeneo husika kwa wakati.

Niwaombe muendelee kushirikiana na Tume ili kuweza kufanikisha jukumu hili lililopo mbele yetu la Uchaguzi Mdogo wa Ubunge na Madiwani.

Baada ya kusema hayo, natamka kuwa mkutano wetu umefunguliwa rasmi.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA